TANGAZO LA SERIKALI Na. 220 la tarehe 15/4/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO YA MWAKA 2022

Jina na Mwanzo wa Kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya bagamoyo ya Mwaka 2022 na itaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, tarazo, moramu, mawe, kokoto, mawe, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

3.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

4. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

5.- (1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

6.- (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

7.- (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

8. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa na adhabu

9.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha kwanza atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili

na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufifilisha kosa

10.- Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali na. 403/2012 la Tarehe 28/12/2012

11.- Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya yaa Bagamoyo, 2012.

*Tangazo la Serikali Na. 220 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

(Chini ya kifungu cha 3(1))

A.Ushuru mbalimbali

| Na | Aina ya Mazao | Kiwanago cha ushuru na kipimo/(kwa kilo1) |
|---|---|---|
| 1 | korosho na mazao ya biashara | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa kilo |
| 2 | Nafaka | 3% ya bei ya mauzo sokon kwa kilo |
| 3 | Samaki na mazao ya samaki | 5% ya bei ya mauzo sokoni kwa kilo |
| 4 | Matunda | 3% ya bei ya mauzo sokoni |
| 5 | Dagaa | 5% ya bei ya mauzo sokoni kwa kilo |
| 6 | Mazao ya mikunde | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa kilo |
| 7. | Unera/mkonge | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa kilo |
| 8. | Ushuru wa nyumba za kulala wageni | 10% ya bei ya chumba kwa siku |
| 9. | Ushuru mkaa | 1,000 kwa gunia |
| 10. | Kuni, kuni, nguzo,gogo,fitomrunda | 1,000 kwa mita za ujazo |
| 11. | Ushuru wa chumvi | Tsh. 200 kwa kg 50 |

B.ushuru wa huduma ya usafi wa Machinjio

| Na | Aina ya mifugo | Kiasi cha ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | Tsh 3,000/= kwa mfugo |
| 2 | Mbuzi | Tsh 1,500/= kwa mfugo |
| 3 | Kondoa/Punda | Tsh 1,500/= kwa mfugo |
| 4 | Nguruwe | Tsh 2,000/= kwa mfugo |

C. Ada ya Ukaguzi wa Nyama

| Na | Aina ya mifugo | Kiasi cha Ada |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | Tsh 2,000/= kwa Mfugo |
| 2 | Mbuzi | Tsh 1,000/= kwa Mfugo |
| 3 | Kondoa | Tsh 1,000/= kwa Mfugo |

*Tangazo la Serikali Na. 220 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Nguruwe | Tsh 2,000/= kwa Mfugo |

D. Ushuru wa Kushusha Mizigo katika Eneo au Soko lolote liliotengwa na Halmashauri

| Na | Aina ya chombo cha usafirishaji | Kiasi cha ushuru |
|---|---|---|
| 1 | uzito wa kuanzia tani 1 – 5 | Tsh 2,000/= |
| 2 | uzito wa kuanzia tani 6 – 10 | Tsh 5,000/= |
| 3 | uzito wa kuanzia tani 11 – 20 | Tsh 10,000/= |
| 4 | uzito wa kuanzia tani 20 – 50 | Tsh 20,000/= |

E Ada ya Kibali.

| Na. | Aina ya kibali | Kiwango cha Ada ya Kibali (tshs). |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa minara ya mawasiliano | Tsh.1,000,000/= kwa mnara |
| 2 | Ujenzi wa nyumba ya biashara | Tsh. 100,000/= kwa nyumba moja |
| 3 | Ujenzi wa Nyumba ya makazi na biashara | Tshs 50,000/= kwa nyumba moja |
| 4 | Ujenzi wa nyumba za makazi | Tshs 30,000/= kwa nyumba moja |
| 5 | Ujenzi wa Ghala, Karakana, gereji au karaka | Tshs 200,000/= kwa jengo |
| 6 | Ujenzi wa kituo cha mafuta | Tshs 1,000,000/= kwa kituo |
| 7 | ujenzi wa Viwanda vidogo vidogo, mashine za kukoboa au kusaga nafaka (mchele, mahindi) | Tshs 500,000/= kwa jengo |
| 8 | Ujenzi wa Nyumba ya ghorofa moja | Tshs 120,000/= kwa jengo |
| 9 | Ujenzi wa Vyuo Binafsi | Tshs 1,000,000/= kwa majengo |
| 10 | Ujenzi wa Shule | Tshs 500,000/= kwa majengo |
| 11 | Ujenzi wa uzio wakati wa kujenga jengo | Tshs 50,000/= kwa uzio |
| 12 | Ujenzi wa Kibanda chochote cha biashara | Tshs 10,000/= kwa kibanda |
| 13 | Ada ya adhabu kwa mtu aliyejenga bila kibali cha ujenzi | Asilimia 3% ya gharama za ujenzi kwa hatua ya ujenzi iliyofikiwa |
| 14 | Tamasha | 50,000/= kwa siku |
| 15 | Michezo | 20,000/=. kwa siku |
| 16 | Ngoma za utamaduni | 20,000/=, kwa siku |
| 17 | Maonyesho ( exhibition) [ya ndani ya nchi] | 20,000/=, banda kwa siku saba |

*Tangazo la Serikali Na. 220 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 18 | Maonyesho ( exhibition) [ya kimataifa] | 500,000/=, tukio zima. |
| 19 | Maombi ya kibali cha kumiliki chimbo la madini ya ujenzi | 1,000,000, kwa mwaka |

G. Ada ya zabuni

| | Aina ya Zabuni | Kiwango cha Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Zabuni ya ujenzi wa majengo, barabara na miundo mbini mingine | Tsh. 100,000/= kwa Zabuni |
| 2. | Zabuni za uwakala mbalimbali | Tsh. 100,000/=, kwa zabuni |
| 3 | Zabuni za ugavi wa huduma | Tsh 70,000/=, kwa Zabuni |
| 4 | Zabuni za ugavi Ndogo | Tsh. 20,000/=, Zabuni |

H. Ada za kukodi mali za Halmashauri

| Na. | Vifaaa | Ada |
|---|---|---|
| 1 | Ukumbi wa Mkutano wa Halmashauri:<br>i. Ukumbi mdogo<br>ii. Ukumbi mkubwa | Tshs 250,000/=, kwa siku moja<br>Tshs. 500,000/=, kwa siku moja. |
| 2 | Maeneo ya wazi/ barabara kwa ajili ya shughuli za promosheni na matangazo ya biashara | Tshs 10,000/ kwa siku |
| 8. | Trekta. | 50,000 kwa ekari 1 |

I. Ushuru wa standi na maegesho katika maeneo mengine ya Halmashauri

| S/NO | AINA YA GARI | USHURU WA STENDI (KWA TRIPU) | USHURU WA MAEGESHO (KWA SIKU) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mabasi | Tsh, 3000/= , kwa tripu | 4,000/= kwa siku |

*Tangazo la Serikali Na. 220 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | /malori | | |
| 2 | Hiace | Tsh, 2,000/= kwa tripu | 2,500/= kwa siku |
| 3 | Taxi | Tsh 1000/= kwa siku | 1,000/= kwa siku |
| 4 | Bajaji | Tsh,1000/= kwa siku | 1,000/=, kwa siku |
| 5 | Magari ya watu binafsi | Tsh. 1000, kwa siku | 3000/=, kwa siku |

J. Ada za vibali vya Mabango/ matangazo ya Biashara

| S/NO | AINA YA TANGAZO | USHURU | UKUBWA | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Matangazo yatakayobandikwa kwenye vibao na kuwekwa kando ya barabara kuu na katika ya mji | Tsh. 10,000/= kwa mabango yasiyowaka taa | Kila ft1 ya mraba | Kwa mwaka |
| | | 20,000/= kwa mabango yanayowaka taa | | |
| 2 | Matangazo ya biashara yanayobandikwa kwenye nyumba ya biashara | Tsh. 5,000/= kwa mabango yasiyowaka taa | Kila ft. 1ya mraba | Kwa mwaka |
| | | Tsh 10,000/= kwa mabango yanayowaka taa | | |
| 3 | Matangazo ya biashara yatakayobandikwa kwenye nyumba za makazi | Tsh. 4,000 | Kila ft 1 ya mraba | Kwa mwaka |
| 4 | Matangazo ya biashara kwa njia ya kipaza sauti | Tsh 50,000/= | Kwa siku moja | Kwa siku |
| 5 | Utangazaji wa biashara{ busness promotion and Music band) | 50,000 | Biahara za ndani | Kwa siku |
| | | 100,000 | Bishara za nje | Kwa siku |
| 6 | Ada ya kibali cha kutengeneza picha jongevu na picha za kawaida kwenye maeneo ya | 100,000 | - | Kwa siku |

*Tangazo la Serikali Na. 220 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Halmashauri kwa makampuni madogo wenye lengo la biashara | | | |
| 7 | Matamasha ya mziki na vibali vya sherehe | Ngoma za jadi 10,000 | | Kwa siku |
| | | Muziki wa dansi na bongo fleva 50,000 | | |
| | | Rusha Roho na Taarab 20,000 | - | |
| 8 | Ada ya usajili wa vikundi vya sanaa na wasanii (25% ya ada ya Basata) | 21,500 | - | Kwa mwaka |
| 10 | Kibali cha kikundi cha sanaa(25% ya ada ya Basata) | 10,000 | - | Kwa mwaka |

K .Ushuru wa madini ya ujenzi

| Na | Aina ya chombo cha usafirishaji | Kiasi cha ushuru kwa tripu |
|---|---|---|
| 1 | uzito wa kuanzia tani 1 – 5 | Tsh 2,000/= |
| 2 | uzito wa kuanzia tani 6 – 10 | Tsh 5,000/= |
| 3 | uzito wa kuanzia tani 11 – 20 | Tsh 20,000/= |
| 4 | uzito wa kuanzia tani 20 – 50 | Tsh 30,000/= |

L. Kodi ya pango na majengo mengine ya Halmashauri.

| S/No | Aina ya Jengo | Kodi ya Pango | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Vibanda ndani ya soko | Tsh.40, 000/= | Kwa mwezi |
| | Vibanda nje ya soko | Tsh.80,000/= | Kwa mwezi |
| 3 | Vibanda ndani ya stendi | Tsh. 100,000/= | Kwa mwezi |
| 4 | Vibanda nje ya stendi | Tsh.50,000/= | Kwa mwezi |

N. ADA ZA HUDUMA ZA ARDHI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya kuchukua fomu ya kiwanja | 20,000/= | Kwa fomu |
| 2 | Upimaji wa shamba | 100,000/= | Kwa ekari moja |
| 3 | Ada ya upimaji (survey) | 20,000/= | Kwa ekari moja |
| 4 | Kurudisha kigingi | 50,000/= | Kimoja |
| 5 | Kuoneshwa mipaka | 30,000/= | Kwa kiwanja kimoja |
| 6 | Kuharibu beacon (faini) | 50,000/= | Beacon moja |
| 7 | Kupitisha michoro ya mipango miji | 20,000/= | Kwa mchoro |
| 8 | Kamisheni ya mauzo ya ardhi kwa | 15% | Kwa bei ya kiwanja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | miradi ya PPP | | |
| 9 | Kamisheni ya kufanya utafiti wa eneo linalotakiwa kununuliwa au kuuzwa | 10% | ya bei ya kiwanja |

O. ADA ZA BOTI /MAJAHAZI

| NA | Urefu wa Boti/Jahazi | Maegesho kwa siku | Ada ya usajiri /leseni |
|---|---|---|---|
| 2 | Mita 1 hadi mita 11 | 500 kwa boti au jahazi | 17,000 kwa mwaka |

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 10)*

KUFIFILISHA KOSA

Mimi……………………………………………..…………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya ..............................., kwamba mnamo tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. za mwaka 2022.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya ya .............................., Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina………………………………………Saini……………………………………

Mbele ya:

Jina……………………………………...Cheo…………………………………….

Saini……………………………………Tarehe……………………………………

*Tangazo la Serikali Na. 220 (Linaendelea.)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kilichofanyika tarehe 17/11/2021.

SHAURI SELENDA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bagamoyo.*

MOHAMED ABDALLAH USINGA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bagamoyo.*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
1 Machi, 2022

INNOCENT L. BASHUNGWA (MB.),
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi,*